JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P. 38
GEITA
Simu: 028-2520004
Nukushi: (028) 2520040
Baruapepe: rbcgeita@pccb.go.tz
Website: www.pccb.go.tz

GEITA – 16 Desemba, 2020.

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

TAKUKURU MKOA WA GEITA YAREJESHA VIUWATILIFU VYENYE THAMANI YA SHILINGI 9,500,000/= VILIVYOCHEPUSHWA KWA AMCOS YA BUKAGA.

YAING'ATA QNET NA KUMREJESHEA MWALIMU SHILINGI 5,480,000/= ALIZODHULUMIWA.

NDUGU WANAHABARI
Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoani Geita imeendelea kutekeleza majukumu yake ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na makosa yanayohusiana kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11/2007. Tukumbuke kuwa "**Rushwa ni mbaya sana kwakuwa hunufaisha mafedhuli kwa hasara ya wengine".**

Ni vizuri wana Geita na Watanzania kwa ujumla wakakumbushwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inahimiza kauli mbiu ya **"HAPA KAZI TU"**. Hivyo kila mmoja wetu atambue kuwa ni lazima afanye kazi halali ili kujipatia kipato halali.

TAKUKURU Mkoa wa Geita katika kutekeleza majukumu yetu tumeweza kubaini matukio ambayo ni vyema umma ukajua.

NDUGU WANAHABARI

Kwanza:

Tumeweza kubaini kuwa kuna kampuni inayojulikana kwa jina la **QNet** inayojihusisha na biashara kupitia mtandao. Kampuni hii imelalamikiwa na Mwalimu aitwaye ROSE FRANK MGIMBA ambaye anafundisha shule ya msingi Lukaranga iliyopo Halmashauri ya Mji Geita baada ya kudhulumiwa kiasi cha shilingi 5,480,000/= kwa njia za ushawishi, kurubuni na kuahidiwa kutengeneza faida ya fedha maradufu baada ya kuwezeshwa kufungua duka mtandaoni.

Baada ya uchunguzi dhidi ya malalaniko hayo, TAKUKURU Mkoa wa Geita imebaini kuwa kampuni hiyo ya QNet inaendesha biashara hiyo bubu mkoani Geita kwa kuwatumia watu wanaojiita wawakilishi huru wa QNet ambao ndio wanaoshawishi na kuwalaghai watu kujiunga katika mtandao wa biashara hii haramu.

Kampuni hii ya QNet haijasajiliwa na Msajili wa Makampuni kufanya biashara na haina Leseni ya biashara hii. Kibaya zaidi kinara na kiongozi wa wawakilishi huru hawa mkoani Geita aitwaye ANETH PHILEMON BIKOMBO anafanya biashara hiyo kupitia mwavuli wa Taasisi yake isiyokuwa ya kiserikali (NGO) aliyoisajili kwa jina la Teknolojia katika maendeleo endelevu (Technologies In Sustainable Development Organization).

Pia miongoni mwa wawakilishi huru ni watumishi wa umma ambao wamekwisha jiunga na mtandao huo ambao ndio wanatumika kuwashawishi watumishi wenzao kujiunga na mtandao huu wa biashara haramu ambao ili uendelee kukua ni lazima kuendelea kusajili wanamtandao.

Kwakuwa mwalimu **ROSE FRANK MGIMBA** alilalamika TAKUKURU uchunguzi umefanyika na ukabaini ni kweli amedhulumiwa kiasi cha shilingi **5,480,000/=** kwa ahadi ya kufunguliwa duka la mtandaoni na mwisho wa siku aliletewa bidhaa ambazo aliambiwa ni kwa ajili ya matumizi yake ya nyumbani na siyo duka na kwamba aendelee kushawishi wateja wengine wajiunge. Katika hali ya kawaida hakuna mwananchi mwenye hali ya kipato cha kawaida anayeweza kufanya manunuzi ya bidhaa ya matumizi ya kawaida kwa gharama kiasi kama hicho cha fedha kwa mkupuo. Kwakuwa wahusika walibanwa wakarejesha fedha hizo walizomdhulumu huyu mwalimu leo anakabidhiwa fedha zake zote shilingi 5,480,000/=.

Wito wa TAKUKURU mkoa wa Geita kwa Wana Geita - watumishi wa umma hasa walimu ni kwamba wajiepushe kujiunga na biashara haramu kama hii wakikumbuka kwamba hakuna njia ya mkato ya kujipatia kipato kikubwa bila kufanya kazi ili kujiepusha na uhalifu wa namna yoyote ikiwemo ukwepaji kodi, Uhujumu uchumi na utakatatishaji wa fedha. Kwa kuwa biashara hii inafanyika kwa njia haramu, TAKUKURU kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Usalama tutaendelea kuwasaka wana mtandao wote mkoani Geita ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria na hatutaruhusu biashara hii kuendelea Mkoani Geita na wananchi wetu kuendelea kudhulumiwa.

NDUGU WANAHABARI

Jambo la pili; Ni katika kutekeleza majukumu yetu ya kawaida kwa mujibu wa sheria, tumeweza kukamata Box 19 za viuwatilifu vya aina ya DUDUBA EC450 zilizokuwa zimetolewa na Bodi ya Pamba kwa ruzuku ya Serikali kwa ajili ya wakulima wa pamba wa AMCOS ya BUKAGA inayojumuisha vijiji viwili vya Bulela na Gamashi katika kata ya Bulela Halmashauri ya Mji wa Geita kwa ajili ya kuua wadudu waharibifu wa Pamba ambazo zilikuwa zimechepushwa na mhasibu wa AMCOS hiyo ambaye jina **limehifadhiwa**.

Dawa hizo zilikamatiwa katika eneo la Nyankumbu Mkoani Geita baada ya kupata **Taarifa za Kiintelijensia** zikiwa zinasafirishwa katika basi la abiria liitwalo KBS lenye namba za usajili T552 ARN kama furushi la mzigo kupelekwa Mkoani Tabora.

Viuwatilifu hivi kila Box lina chupa 100 ambapo thamani ya kila chupa kwa ruzuku ya Serikali ni shilingi 2,000/= na bei yake sokoni bila ruzuku ya Serikali ni shilingi 5,000/=. Unaweza kuona hasara iliyokuwa imesababishiwa Serikali ambayo ni shilingi 9,500,000/=.

Kwakuwa uchunguzi unaendelea, ikumbukwe kwamba viuwatilifu hivi vina muda wake wa matumizi (Expiring Date) na wananchi wana uhitaji wake mkubwa kwani jitihada za Serikali ni kuhakikisha kilimo cha zao la pamba kinakuwa endelevu. Hivyo leo hii ninakibidhi viuwatilifu hivi kwa mwakilishi wa Bodi ya Pamba ili viweze kugawiwa kwa wakulima wanachama wa AMCOS ya BUKAGA kama ilivyokusudiwa awali na Serikali baada ya taratibu za mahakama kukamilishwa.

Wito wa TAKUKURU mkoa wa Geita kwa watumishi wa umma na viongozi wa AMCOS zote mkoani Geita kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia misingi ya uadilifu na kujali maslahi ya umma na siyo maslahi binafsi, kwani kwa

kitendo hiki kilichofanyika ni uhujumu uchumi na kinakwamisha juhudi za Serikali kuwakwamua wakulima wa zao la pamba nchini. Natoa tahadhari na kwa wengine wenye nia ya kujihusisha na vitendo vya rushwa kama hivi ndani ya mkoa wetu, kuacha mara moja la sivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Aidha wananchi wa mkoa wa Geita, waendelee kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa, kuwa waadilifu kwa kutojihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa, washiriki pia kutoa taarifa za vitendo vya rushwa TAKUKURU kwa kupiga simu ya bure 113, *113# au kutuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba 113 au kupitia TAKUKURU APP.

Sote Tuseme *"KUPAMBANA NA RUSHWA NI JUKUMU LANGU"*

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA

IMETOLEWA NA:
Leonidas R. Felix
MKUU WA TAKUKURU (M) GEITA